

# **Kujenga Upya Kalenda za Kilimo Kupitia Fikra za Mifumo Hai**

Jackson Kithokilo (Mkulima na Mwalimu wa Kilimo  
Rejeshi)- ECHO Webinar, 11 Novemba 2025

## Kujenga upya kalenda za kilimo kwa kutumia fikira za mifumo hai

11 novemba 2025  
14:00 CAT (15:00 EAT)  
mkutano wa  
mtandaoni  
bila malipo  
**Jackson Kithokilo**



*Mkulima mwenye uzoefu na  
anayefanya kilimo cha kurejesha ardhi  
na Mtaalamu katika Afrika Mashariki*



# Kusikiliza Saa ya Ardhi

- ▶ Muda katika kilimo ni hai na rejeshi, si wa kimitambo.
- ▶ Ukiwa mtoto, ulijuaje kuwa mvua inakaribia?
- ▶ Washiriki hushiriki ishara kama maua ya miti, vyura, upepo, nyota, mwezi.
- ▶ Wazee wetu hawakuhesabu siku; walihesabu ishara za upya wa maisha.



# AFRIKA MASHARIKI



- Misimu yote inategemeana.
- Kila msimu unamazao unaokuza na nguvu ya asili inayorejeshwa kwa ardhi .
- Misumu yote inasapoti maisha na kilimo hai/rejeshi.



# Hekima za Kanda za Afrika Mashariki

KE - Akamba: Ndege Mwanzia na maua ya Mutunguu yalitabiri mvua fupi (Vuli).

TZ- Wachagga & Wameru: Ukungu wa Kilimanjaro = wakati wa kupanda ndizi na maharage.

UG- Bagisu: Tohara na msimu wa kupanda = upya wa ardhi na roho.


DRC- Luba: Wakati Nkulu (Jamii ya mkuyu) unapozaa matunda, ni wakati wa kupanda mihogo.

# Fikra za Mifumo Hai

- ▶ Mifumo hai ni mtazamo unaoona dunia kama kiumbe kinachopumua.
- ▶ Udongo = tumbo
- ▶ Maji = damu
- ▶ Miti = mapafu
- ▶ Mizizi = mishipa
- ▶ Mkulima = akili
- ▶ Tunapounganisha vipengele hivi, tunaunda shamba lenye uhai na urejeshi.
- ▶ ***Tunapotenganisha udongo na mvua, au miti na mazao, tunavunja mwili wa ardhi. Mkulima mwenye fikra za mfumo hai hulima kwa uhusiano – si kwa mgawanyiko.***

# Fikra za Mifumo Hai ni Nini?

Ni mtazamo unaoona dunia kama kiumbe hai kinachopumua.

 Wakulima wa kale walifuata ishara za asili kama mwezi, ndege, upepo, na maua.

Hekima hii inaweza kutuongoza leo kurejesha urari wa kilimo.



# **Kurejsha Kalenda hai na za Asili za Kiafrika**

**Mada Kuu:** Kabla ya kalenda za kikoloni, jamii za Kiafrika zilifuata kalenda za kiikolojia, za angani na kijamii ,zenye mapigo ya asili,uhai na urejeshi.

**Labda tuwaze :**

**...Wazee wenu walijuaje wakati wa kupanda, kuvuna, au kuhamia?**

- ▶ **Hadithi Fupi:**
- ▶ Mkulima wa Uganda anapoona vyura wamerudi, si ushirikina – ni ishara ya uhai wa vijidudu ardhini na kurudi kwa maji. Sayansi inathibitisha hekima hii.
  
- ▶ **Mawazo ya Kisasa:**
- ▶ **Dijitali + Asili:** Kuunganisha programu za mwezi na utabiri wa wazee.
- ▶ **Viashiria Hai:** Kufuatilia magugu (mf. *nut grass*, *gugu karoti*) kuelewa rutuba na unyevu wa udongo.
- ▶ Kuunda kalenda za urithi wa mazao kwa kufuata mzunguko wa misitu.
- ▶ **Kilimo cha Kulingana na Mwezi:** Kupanda mazao yenye majani kwenye mwezi unaokua, na mizizi kwenye mwezi unaopungua.

Tabia za Kalenda inayotumia  
fikra za mifumo hai na rejeshi


# 1. UUNGANISHO (Interconnectedness)

- ▶ Kila kitu kimeunganishwa - udongo, maji, mimea, watu.
- ▶ Mfano: Wachagga walitumia mawingu ya Mlima Kilimanjaro kutabiri mvua.
- ▶ *Tunapopanda kwa uhusiano, tunapanda kwa usawa, si kwa haraka.*



## 2.MZUNGUKO NA MREJESHO (Circularity & Feedback)


- ▶ Kila mwisho ni mwanzo mpya.
- ▶ Mfano: Wanasukuma walipumzisha ardhi baada ya mavuno ili kujirejesha.
- ▶ Urejeshaji ni mduara wa maisha, si tukio la msimu mmoja.







## 3. UWEZO WA KUBADILIKA (Adaptability & Learning)

- ▶ Mifumo hai hubadilika na kujifunza kutokana na mazingira.
- ▶ Mfano: Wakamba walibadilisha kutoka mahindi kwenda mtama kutokana na ukame.
- ▶  Kadri tunavyoangalia, ndivyo ardhi inavyotufundisha.




## 4. KUJENGWA KATIKA NGUZO (Nestedness)

- ▶ Kila mfumo upo ndani ya mwingine: mmea → *udongo* → *ikolojia* → *hali ya hewa* → *dunia*.
- ▶ Mfano: Wakulima wa Kongo walipanga upandaji kulingana na kupanda kwa maji ya mito.
- ▶ Tukipatana na mizunguko mikubwa ya dunia, muda unakuwa hekima.



## 5. TOFAUTI NA USHIRIKIANO (Diversity & Co-operation)

- ▶ Utofauti huleta uimara.
- ▶ Mfano: Waganda walitumia ishara za ndege, wadudu, na mwezi kupanga upandaji.
- ▶  Kadri tunavyosikiliza sauti nyingi za maumbile, ndivyo tunavyoelewa muda vizuri zaidi.





## 6. USHIRIKIANO NA UREJESHAJI (Reciprocity & Regeneration)

- ▶ Ardhi hutupa; nasi tunapaswa kurudisha.
- ▶ Mfano: Wamaasai walipanda miti baada ya msimu wa malisho.
- ▶ Ardhi hutoa tunapojifunza kutoa pia.



## 7. UKAMILIFU NA MAANA (Wholeness & Purpose)

- ▶ Kalenda za kilimo ziunganishe chakula, afya, na roho.
- ▶ Mfano: Wamijikenda walifanya tambiko za mvua kabla ya kupanda. Wakristu hufanya maombi kabla ,baada ya mvua na mazao. Pia hutoa zaka.
- ▶ Kupima muda ni kulinda uhai.

## Labda Tujiulize ?

- ▶ Ni sifa gani ya mfumo hai unaiona ikifanya kazi kwenye ardhi /shamba yako leo?'
- ▶ 'Tukijenga upya kalenda, tunajenga upya uhusiano wetu na maisha.'
- ▶ 'Wakati ardhi inazungumza, mkulima mwenye hekima hupanda.'

# Shamba kama Kiumbe Hai

- ▶ Kila shamba lina mapigo ya moyo yake.
- ▶ Tambua mianya 2 ya nishati: mmomonyoko, taka, kupoteza virutubisho.
- ▶ Tambua vianzilishi 2 vya uhai: mbolea hai, uvunaji maji, ushirikiano.

# Tafakari

- ▶ Swali: Ni nini utasikiliza kwenye ardhi yako kuanzia leo?
- ▶ 'Tunapolingana na midundo ya asili, kalenda zetu zinakuwa nyimbo za uhusiano.'
- ▶ *Ardhi inapozungumza, mkulima mwenye hekima hupanda.* – *Methali ya Afrika Mashariki*



***Tazama → Tafakari →  
Chukua Hatua →  
Rejeshha'***